**HOTUBA YA MHE. DKT. TITUS MLENGEYA KAMANI (MB) WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI KWENYE UZINDUZI WA BARAZA LA TATU LA MWAKA LA WADAU WA TASNIA YA NYAMA ULIOFANYIKA KWENYE UKUMBI WA HOTELI YA GLONECY MOROGORO, TAREHE 15 APRILI, 2015**

**Mhe. Dr. Rajabu Retengwe, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro,**
**Dkt. Yohana L. Budeba, Katibu Mkuu, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi,**
**Bibi. Doreen Maro, Mwenyekiti wa Baraza la Mwaka la Wadau wa Tasnia ya Nyama,**
**Dr. Sikubwabo Ngendabanka, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Nyama Tanzania,**
**Ndugu Wawakilishi wa Wizara na Taasisi za Serikali,**
**Ndugu Wawakilishi wa Taasisi zisizo za Kiserikali (NGO),**
**Ndugu Wajumbe wa Baraza la Mwaka la Wadau wa Tasnia ya Nyama,**
**Ndugu Wajumbe wa Bodi ya Nyama Tanzania,**
**Wageni Waalikwa,**
**Wanahabari,**
**Mabibi na Mabwana.**

Awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutukutanisha leo hapa katika siku hii muhimu tukiwa na afya njema. Siku ya leo ni ya kihistoria kwangu kwani ni mara ya kwanza kukutana na wadau wa Baraza la Mwaka la tasnia ya nyama tangu nilipoteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete Januari, 2014 kuongoza Wizara hii. Aidha, nachukua fursa hii kuushukuru uongozi wa Mkoa wa Morogoro kwa kukubali kuwa wenyeji wa mkutano huu kwa mara nyingine na mapokezi mazuri kwa wadau wote waliohudhuria katika mkutano huu.

**Ndugu Mwenyekiti**, Napenda kukupongeza wewe mwenyewe na wajumbe wote wa Baraza hili kwa kuteuliwa kwenu kuiongoza tasnia ya nyama kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo. Aidha, nitumie fursa hii pia

kuzipongeza Wizara, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Vyama vya Wadau zilizowezesha wajumbe kushiriki katika mkutano huu wa kisheria na muhimu katika maendeleo ya tasnia ya nyama, wenye kauli mbiu isemayo ***"Vyama vya Wadau Imara ni Nguzo kwa Maendeleo ya Tasnia ya Nyama".*** Kwa kuzingatia idadi ya wadau waliohudhuria, nashawishika kusema kwamba mmehamasika na mnafahamu kwamba jukumu la kuendeleza sekta ya mifugo na tasnia ya nyama hapa nchini ni la wadau wenyewe na ushiriki wenu ni muhimu katika kufikia lengo hilo.

**Ndugu Mwenyekiti**, Nimeambiwa kwamba Baraza hili linazinduliwa likiwa na wajumbe takriban **110** wanaowakilisha wadau kutoka katika Wizara mbalimbali, Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara, Taasisi mbalimbali, Mashirika yasiyo ya Kiserikali na Vyama vya Wadau kitaifa, yaani wafugaji (CCWT), wafanyabiashara (TALIMETA) na wasindikaji (TAMEPA). Kupendekezwa kwenu kuwa wawakilishi wa wadau wa tasnia ya nyama kutoka katika taasisi zenu inaonesha imani iliyojengeka kwenu kutoka kwa viongozi wenu. Ni vyema mkaelewa kuwa mmepewa dhamana kubwa ya kuwezesha mabadiliko chanya katika tasnia ya nyama ili kuongeza mchango wake katika uhakika wa chakula, kipato cha familia na Pato la Taifa kwa ujumla. Hivyo ni matumaini yangu kuwa mtatumia weledi wenu na uzalendo katika kuchangia upatikanaji wa maendeleo ya haraka na kuibadilisha taswira ya tasnia ya nyama ili tuweze kwenda na kasi ya mabadiliko ya sayansi yaliyopo hivi sasa duniani kote.

**Ndugu Mwenyekiti**, maendeleo ya tasnia hii yatewezekana tu endapo tutafanikiwa kuongeza tija katika uzalishaji kwa kuwa na mifugo yenye kosaafu bora inayoweza kukua kwa haraka na kufikia uzito unaostahili kupelekwa sokoni katika kipindi kifupi tofauti na ilivyo hivi sasa. Baraza hili lina nafasi kubwa ya kusaidia kubadilisha fikra (*mindset*) za wafugaji wetu ili kuweza kuendana na mabadiliko na kuacha utamaduni wa kufuga mifugo mingi ambayo haina tija na kuwafanya waendelee kuwa watumwa wa mifugo yao. Mkiwa kama wadau muhimu wa sekta hii mnajukumu la kuishauri Serikali namna bora zaidi ya kusimamia tasnia ya nyama ili

kuweza kufikia malengo ya kuhakikisha kuwa tasnia ya nyama inaongeza mchango wake katika Pato la Taifa na kuongeza utajirisho kwa wadau wa sekta.

Nina imani kuwa mtazitumia vizuri siku mbili za mkutano huu kujadili kwa kina changamoto zinazoikabili tasnia ya nyama na kuweka mikakati ya kutumia changamoto hizo kama fursa ili tuweze kutoka hapa tulipo. Napenda kuwaahidi kuwa Wizara yangu iko tayari kufanyia kazi mapendekezo na maazimio mtakayofikia mwisho wa mkutano huu ili kuleta mabadiliko ya haraka.

**Ndugu Mwenyekiti,** Imekuwa kawaida yetu kila tunapokutana kujivunia takwimu za wingi wa mifugo tuliyo nayo Tanzania, nadhani sasa ni wakati mwafaka wa kubadilisha mazoea haya na kuzungumzia namna ambayo mifugo hiyo inanufaisha watanzania na Taifa kwa ujumla. Hivyo, hatuna budi kujitathimini uwezo wetu wa kutumia rasilimali hii kubwa ya mifugo ikiwa ni takriban ng'ombe milioni **22.8**, mbuzi milioni **15.6**, kondoo milioni **7.0**, kuku wa asili milioni **35.5**, kuku wa kisasa milioni **35.5** na nguruwe milioni **2.01.** Pamoja na fursa ya soko la nje vilevile, kuna haja ya kuhamasisha ulaji wa nyama nchini ikizingatiwa kuwa takwimu zinaonesha kuwa ulaji wa nyama ni kilo **12** kwa mtu kwa mwaka ikilinganishwa na kiwango cha kilo **50** za nyama kwa mtu kwa mwaka kilichopendekezwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO). Hebu tujiulize ndugu zangu, kiasi hiki kinatosha, tatizo ni nini na tunawezaje kuongeza ulaji huu?

**Ndugu Mwenyekiti**, Kwa upande mwingine, miundombinu ya kuwezesha biashara ya nyama ndani ya nchi hususan machinjio zilizoko katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hazikidhi viwango vya kuzalisha nyama bora na salama vinavyohitajika na baadhi ya walaji wa ndani kwa mfano mahoteli ya kitalii, migodi na *supermarkets.* Hali hii inafanya nchi ilazimike kuingiza nyama nyingi kutoka nje ya nchi ambapo kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014 takriban tani **2,000** za nyama ziliingizwa nchini. Ili kuondokana na hali hii ni vyema Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa

zikaweka kwenye bajeti zake pamoja na kutafuta fedha kutoka katika vyanzo vingine ili kujenga machinjio za kisasa kwa lengo la kuilinda afya ya mlaji na kutumia fursa ya soko lililopo katika mahoteli ya kitalii, migodi na maduka makubwa (*supermarkets*).

**Ndugu washiriki,** Imefika wakati sasa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazoendesha machinjio kuangalia uwezekano wa kubinafsisha au kuingia ubia katika uendeshaji wa machinjio ili kuweza kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya Mwaka 2003, Sheria ya Nyama Na. 10 ya Mwaka 2006, Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na 18 ya Mwaka 2008, Sheria ya Biashara ya Ngozi Na. 18 ya Mwaka 2008, Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama Na. 13 ya Mwaka 2010, Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo Na. 12 ya Mwaka 2010 na Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Na. 1 ya Mwaka 2003. Sheria hizi zikisimamiwa kikamilifu zitawezesha kudhibiti magonjwa, kuzalisha nyama bora na kupata chakula salama kwa walaji wa ndani na hatimaye nyama yetu kupenya kwenye soko la kimataifa yenye faida kubwa. Jambo kubwa hapa ni dhamira ya dhati kwa wahusika kwenye kuleta mabadiliko yanayohitajika.

**Ndugu Mwenyekiti**, Kwa namna ya kipekee kabisa napenda kuwashukuru wafugaji wa asili kwa kuendeleza ufugaji licha ya changamoto zinazowakabili. Hii ni kutokana na ukweli kwamba tariban asilimia **98** ya takwimu za mifugo nilizozitaja awali inachangiwa na mifugo kutoka katika kundi hili la wafugaji. Baadhi ya changamoto zinazowakabili ni upatikanaji wa ardhi ya ufugaji na miundombinu yake, migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardí ambayo wakati mwingine husababisha vifo vya watu na mifugo, kuwa na mbegu bora za mifugo, kuwa na teknolijia bora za uzalishaji, kinga na tiba za mifugo, ufuatiliaji wa mifugo na mazao yake, kuwa na muundo imara (kwa kuwa na vyama vya wadau) na kutokidhi mahitaji ya soko kutokana na udhaifu wa muundo wa uendeshaji na ufinyu wa mitaji. Ni dhahiri kwamba uwekezaji katika kutatua changamoto zinazokabili ufugaji wa asili utaleta mabadiliko

makubwa na ya haraka. Hivyo, nihimiza wadau wote wanaohusika na maendeleo ya sekta ya mifugo kujikita katika kutatua changamoto za wafugaji hawa ili kuongeza kipato chao na cha Taifa kwa ujumla. Aidha, ninawahimiza wafugaji kusajili mifugo yao kwa ajili ya ufuatiliaji wa mazao ya mifugo, pamoja na kujisajili wao wenyewe ili kazi zao zitambuliwe na kuhusishwa kikamilifu katika masuala yanayohusu maendeleo ya tasnia.

**Ndugu Mwenyekiti,** Kwa sababu hizo hizo nilizozitaja hapo juu, nimeambiwa kwamba Wadau wa Ukanda wa Afrika ya Kaskazini na Mashariki kutoka katika nchi **13** za Burundi, Djibouti, Jamhuri ya Demokrasia Congo (DRC), Eritrea, Ethiopia, Misri, Kenya, Rwanda, Somalia, Sudan Kusini, Sudan, Uganda na Tanzania, chini ya ufadhili wa AU-IBAR na IGAD wameunda Chama cha Wadau wa Sekta ya Mifugo kinachojulikana kama "Baraza la Wadau wa Mifugo Ukanda wa Kaskazini na Mashariki ya Afrika" [NEALCO]. Lengo la Chama hiki ni kuhamasisha, kuratibu, kutafuta na kupeana taarifa na kufanya ushawishi ili kuwezesha biashara ya mifugo na bidhaa zake ndani na nje ya Ukanda pamoja na kufanya majukumu mengine kwa niaba ya wanachama wake ambao ni vyama vya wadau vya Wafugaji, Wafanyabiashara na Wasindikaji kitaifa. Kujiunga katika Vyama kunasaidia kufanya ushawishi na utetezi wa masuala ya kisera na kisheria, kukidhi mahitaji na kuhudumia soko lolote, kupata mbegu bora za mifugo na kupata teknolojia mbalimbali za uzalishaji kwa pamoja na urahisi wa kupata mikopo kutoka katika taasisi za kifedha. Hivyo ninahimiza vyama vya wadau nchini kufanyakazi kwa karibu na Bodi ya Nyama kuweza kunufaika na uanzishwaji wa chama cha NEALCO kutokana na soko la pamoja linaloendelezwa na chama hiki.

**Ndugu Mwenyekiti,** Napenda kuwahakikishia wajumbe wa Baraza hili kuwa fursa ya soko la mifugo na nyama ndani na nje ya Afrika ni kubwa sana, hususan nchi za Afrika ya Kati (Jamhuri ya Demokrasia (DRC), Rwanda, Burundi na Zambia); Afrika ya Kaskazini (Djibouti, Misri) na nchi za Mashariki ya kati hususan Falme za Kiarabu na Oman. Kwa mfano, hivi karibuni nchi yetu ilipata soko la nyama ya mbuzi kiasi cha tani **5,000** na nyama ya ng'ombe tani **1,000** kwa wiki kwenda nchi ya Misri na Dubai.

Soko hili limetushinda kulihudumia kutokana na uzalishaji wa mmoja mmoja na kutegemea machinjio moja kwa ajili ya kuuza nje. Ninaamini kwamba changamoto hii inaweza kutatuliwa endapo vyama vya wadau vitajiimarisha na kulenga biashara ili kukidhi mahitaji ya ubora, uzito na muda wa soko. Hivyo, ninaagiza vyama vyote vya wadau katika ngazi ya kitaifa kujiimarisha kwa mujibu wa katiba zao na kuwa na mpango mkakati wa kutekeleza majukumu ya vyama yao hususan mchango wa vyama katika kukuza biashara ya mifugo na bidhaa zake.

**Ndugu Mwenyekiti,** Kwa mujibu wa Sheria ya Nyama Na. 10 ya Mwaka 2006, mkutano huu wa Baraza hutekeleza majukumu yake Kisheria ikiwa ni pamoja na:

a. Kuhamasisha maendeleo endelevu ya tasnia ya nyama Tanzania;
b. Kupokea na kuchambua taarifa mbalimbali za Bodi ya Nyama Tanzania;
c. Kupendekeza wajumbe wa Bodi kwa ajili ya kuteuliwa na Waziri;
d. Kumshauri Waziri pamoja na Bodi kuhusu masuala ya maendeleo ya tasnia ya nyama na mambo yanayojitokeza wakati wa kutekeleza Sheria hii; na
e. Kufanya kazi nyingine yoyote kama itakavyohitajika katika utekelezaji wa Sheria hii.

Mtakubaliana na mimi kwamba utekelezaji wa majukumu yaliyoainishwa katika kifungu (b), (c), na (d) hapo juu yanahitaji umakini mkubwa. Hivyo, napenda kusisitiza kwamba wakati wa kupendekeza majina matatu ya wajumbe kutoka katika makundi ya Wafugaji, Wafanyabiashara ya Mifugo na Nyama, Wasindikaji, Wafanyabiashara ya pembejeo za mifugo na Walaji kwa ajili ya kuteuliwa kuingia katika Bodi ya Nyama Tanzania mzingatie sifa stahiki yaani weledi, uzoefu, maono chanya yanayozingatia mazingira ya sasa ya utandawazi katika uchumi wa soko na ushindani wa kibiashara ili kuendeleza tasnia ya nyama. Bodi ya Nyama Tanzania ni chombo tendaji cha kusimamia maendeleo ya tasnia hii na inaundwa na wadau wenye uchungu na tasnia, pia, ni vizuri tutambue kwamba kazi ya Serikali ni kuwawezesha wananchi kuanzisha vyombo vyao ambavyo vitabeba

dhamana ya kuendeleza sekta. Baraza linahimizwa kujadili namna bora ya kujiendesha na kuwezesha maendeleo ya tasnia ya nyama nchini.

**Ndugu Mwenyekiti,** Narudia tena kusema kuwa maendeleo ya tasnia ya nyama yanategemea hamasa ya wananchi katika kubadilika na kuanza kufuga kisasa na kibiashara. Serikali kwa upande wake itaendelea kuweka mazingira mazuri kisera na kisheria ili kuongeza ufanisi na tija. Ni matumaini yangu kwamba Baraza hili litajadili kwa kina na hatimaye kuweka mikakati ya kupunguza au kuondoa kabisa changamoto zinazoikabili tasnia, kuendeleza soko la nyama, na hivyo kuongeza mchango wa sekta ya mifugo hususan tasnia ya nyama kwenye Pato la Taifa.

**Ndugu Mwenyekiti, Wajumbe wa Baraza, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mbwana,** Ninawatakia mkutano mwema wenye ufanisi na mafanikio. Baada ya kusema hayo**,** napenda kutamka kuwa Baraza la Tatu la Mwaka la Wadau wa Tasnia ya Nyama **LIMEZINDULIWA RASMI** na mkutano wa sita **UMEFUNGULIWA RASMI.**

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA**